



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Thelathini na Moja – Tarehe 09 Juni, 2022

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

88. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali amekuwa akiendelea kuishauri Serikali kupitia Ripoti zake kutokana na dosari mbali mbali anazozibaini, na kwa kuwa Taasisi nyingi zimeonekana kuendelea kutotii ushauri huo kwa maendeleo ya nchi.

Je, Serikali imechukuwa hatua gani kwa wale wote waliobainika kusababisha hesabu zao kutoonesha sura sahihi na halisi.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

127. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Serikali inastahili pongezi kwa mpango wake wa kuleta boti kwa ajili ya kuimarisha usafiri salama kati ya visiwa vikubwa na vidogo vidogo Unguja na Pemba. Hata hivyo, tathmini ya wananchi inaonyesha kutofikiwa kwa ufanisi bora na malengo ya mpango huo.

- (a) Je, ni boti ngapi na kwa gharama zipi zimenunuliwa na Serikali kwa ajili ya kuimarisha usafiri salama kuelekea visiwa vidogo vidogo ndani ya Zanzibar.
- (b) Je, boti hizo zimeanza kutumika kama ilivyokusudiwa na kwa utaratibu upi.
- (c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuishirikisha sekta binafsi katika huduma hii ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi.

Wizara ya Afya:

171. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Ni jambo jema kwamba, Serikali ina utaratibu maalum wa kutoa ruhusa kwa watumishi wake kwenda kusoma zaidi ili kuongeza sifa na weledi unaohitajika katika kazi husika sambamba na kutimiza masharti ya muda wa kuwepo kazini na uwepo wa wafanyakazi wa kutosha katika fani na nafasi ambayo mtumishi anaenda kusoma anaifanyia kazi. Hata hivyo, kumekuwa na ubaguzi uliokithiri katika kutoa ruhusa hizo, hasa zaidi katika Wizara ya Afya, huku utaratibu, masharti na kanuni zikiwekwa upande kwa baadhi ya wafanyakazi wanaopendelewa na visingizio vya kutengeneza vikitumika kuwakosesha wengine haki zao ambao wako tayari na wana wadhamini.

- (a) Je, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ni wafanyakazi wangapi wa Wizara ya Afya wameruhusiwa kwenda kusoma na wangapi hawakuruhusiwa.
- (b) Je, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, ni wafanyakazi wangapi wa Wizara ya Afya walioruhusiwa kwenda

kusoma bila sifa ya kuruhusiwa na wangapi wasioruhusiwa ambao wana sifa.

- (c) Je, ni upi mpango wa ruhusa ya masomo wa mwaka 2022/2023 kwa wafanyakazi wanaotaka kujiendeleza na wenye sifa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

161. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Umoja wa Mataifa umetangaza rasmi kuitambua lugha yetu adhimu ya kiswahili kuwa miongoni mwa lugha 7 zinazotambuliwa rasmi duniani.

- (a) Kuna vyuo vikuu vingapi duniani vinafundisha lugha ya kiswahili pamoja na idhaa ngapi za redio zinatangaza kwa lugha ya kiswahili duniani.
- (b) Kwa kiwango gani walimu wetu waliobobea na kuhitimu vizuri lugha ya kiswahili wananufaika na fursa za ajira katika taasisi hizo.

II. UCHAGUZI WA MWENYEVITI WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR.

Zanzibar,
09 Juni, 2022.


(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA